jumba lenye vyumba vingi	'a building with/having many rooms'

Fill in the blanks orally:

mji _enye majumba __ngi	mji wenye majumba mengi	a city with many buildings
miji _enye majumba __ngi	miji yenye majumba mengi	cities with many buildings
miji _enye unyevunyevu ___ngi	miji yenye unyevunyevu mwingi	cities with a lot of humidity
nchi _enye unyevunyevu __ngi	nchi yenye unyevunyevu mwingi	a country with a lot of humidity
nchi _enye joto __ngi	nchi yenye joto jingi	a country with a lot of heat
mji _enye joto __ngi	mji wenye joto jingi	a city with a lot of heat
mji _enye mvua ___ngi	mji wenye mvua nyingi	a city with a lot of rain

CYCLE 57

M-1

senema (9)	Unataka kwenda senema?	movies	Do you want to go to the movies?
mji	Unataka kwenda mjini?	town	Do you want to go to town?
______ (jina la ______ jumba)	Unataka kwenda ______?	______ (name of ______ building)	Do you want to go to ______ ? (name of building)
chumba cha kulia	Unataka kwenda chumbani mwa kulia?	dining hall	Do you want to go to the dining hall?

M-2

la	La, sitaki kwenda senema sasa.	no	No, I don't want to go to the movies now.
hebu	Ndiyo, hebu twende.	to like	Yes, let's go.
zetu	Ndiyo, twende zetu!	ours	Yes, let's go!

C-1

Unataka kwenda ______?	Do you want to go ______?
Ndiyo, twende zetu.	Yes, let's go.
au	or
La, sipendi kwenda ______ sasa.	No, I don't want to go to ______ now.

CYCLE 58

M-1

duka	Nitakwenda dukani adhuhuri.	store	I'm going to go to the store at noon.
darasa	Nitakwenda darasani saa saba mchana.	class	I'm going to go to class at 1:00.
mji	Nitakwenda mjini saa kumi jioni.	town	I'm going to go to town at 4:00.
senema	Nitakwenda senema saa mbili usiku.	movies	I'm going to go to the movies at 8:00 p.m.

M-2

saa ngapi?	Utakwenda mjini saa ngapi? (Saa ngapi utakwenda mjini?)	what time?	What time are you going to go to town?

M-3

pamoja	Hebu twende mjini pamoja.	together	Let's go to town together.

C-1

A: Unataka kwenda (mjini)?	A: Do you want to go to (town)?
B: Utakwenda (mjini) saa ngapi?	B: What time are you going to go to (town)?
A: Nitakwenda saa (saa mbili).	A: I'm going at (eight o'clock).
B: Vema. Hebu twende pamoja.	B: All right. Let's go together.

Review daily action chain in relation to plans for tomorrow.

C-2

A: Utaamka saa ngapi kesho?	A: What time are you going to get up tomorrow?
B: Nitaamka saa (moja).	B: I'm going to get up at (seven) o'clock.
A: Utakula chakula cha asubuhi saa ngapi kesho?	A: What time are you going to eat breakfast tomorrow?
B: Nitakula chakula cha asubuhi saa (mbili).	B: I'm going to eat breakfast at eight (o'clock).

CYCLE 59

M-1

kwenda	Utakwenda wapi leo jioni?	to go	Where are you going to go this evening?
kufanya	Utafanya nini leo jioni?	to do	What are you going to do this evening?
kutaka	Unataka kufanya nini leo jioni?	to want	What do you want to do this evening?

M-2

kwenda	Siendi popote leo jioni.	to go	I'm not going to go anywhere this evening.
kufanya	Sitafanya jambo lolote leo jioni.	to do	I'm not going to do anything this evening.
kutaka	Sitaki kwenda popote leo jioni.	to want	I don't want to go anywhere this evening.
kujua	Sijui.	to know	I don't know.
kudhani kufikiri	Sidhani. Sifikiri.	to think	I don't think so.

C-1

A:	Utafanya nini leo jioni?	A:	What are you going to do this evening?
B:	Sijui. Unataka kwenda (senema)?	B:	I don't know. Do you want to go to (the movies)?
A:	Sidhani. Twende (mjini).	A:	I don't think so. Let's go to (town).
B:	Vema. Tutakwenda (mjini).	B:	All right. We'll go to (town).

C-2

A:	Twende (senema) leo jioni.	A:	Let's go to (the movies) this evening.
B:	Vema. Tutakwenda saa ngapi?	B:	All right. What time shall we go?
A:	Twende saa (kumi na mbili jioni).	A:	Let's go at (six p.m.).
B:	La. Sitaki kwenda saa (kumi na mbili).	B:	No, I don't want to go at (six) o'clock.
	Twende saa (moja usiku).		Let's go at (seven p.m.).
A:	Vema. Tutakwenda (senema) saa (moja).	A:	All right. We'll go to (the movies) at (seven).

The next time you plan to go off the campus with one or more fellow students, make the arrangements in Swahili.

You should also describe your own planned activities for the following day (days) and tell the time of day at which you plan to do them.

TO THE STUDENT:

/leo/ 'today' plus /jioni/ 'evening' is translated as 'this evening' just as /mwezi/ 'month' plus /kesho/ 'tomorrow' is translated as 'next month' (Cycle 51).

The stem /-o-ote/ means 'any at all'. When it has the locative prefix /p/, it is translated as 'anywhere'. When it follows a noun, it takes the concordial prefixes required by that noun.

CYCLE 60

M-1

saa	Tunakaa darasani kwa muda wa saa tatu kila asubuhi.	hours	We stay in class for a period of three hours every morning.
miezi	Tutakaa hapa kwa muda wa miezi mitatu.	months	We're going to stay here for a period of three months.
miaka	Tutakaa katika Afrika ya Mashariki kwa muda wa miaka miwili.	years	We're going to stay in East Africa for a period of two years.

M-2

kujifunza	Nilijifunza kilimo kwa muda wa miaka minne.	to study	I studied agriculture for a period of four years.
kuishi	Niliishi Florida kwa muda wa miaka mitano.	to live	I lived in Florida for a period of five years.
kuhudhuria	Nilihudhuria Chuo cha Walimu cha Dudley J. Trudge kwa muda wa miaka sita.	to attend	I attended Dudley J. Trudge College for Teachers for a period of six years.
kubaki	Nilibaki mjini New York kwa muda wa siku sita.	to remain	I remained in New York City for a period of six days.

C-1

A: Unakaa darasani kwa muda gani kila asubuhi?	A: How long do you stay in class every morning?
B: Tunakaa darasani kwa muda wa saa _____________.	B: We stay in class for a period of ____________ hours.

C-2

A: Je, unakwenda (Malawi)?	A: Are you going to (Malawi)?
B: La, siendi (Malawi).	B: No, I'm not going to (Malawi).
Ninakwenda (Kenya).	I'm going to go to (Kenya).
A: Unakwenda (Tanzania), sivyo?	A: You're going to go to (Tanzania), are you?
Utakaa kwa muda gani (Tanzania)?	How long are you going to stay in (Tanzania)?
C: Nitakaa (Tanzania) kwa muda wa (miaka miwili).	C: I'm going to stay in (Tanzania) for a period of (two years).

C-3

A: Unafanya kazi gani?	A: What kind of work do you do?
B: Mimi ni (mwuguzi).	B: I'm a (nurse).
A: Ulijifunza wapi (kuuguza)?	A: Where did you learn (nursing)?

B:	Nilijifunza (kuuguza) katika (Chuo cha Dudley J. Trudge).	B:	I learned (nursing) at (Dudley J. Trudge College).
A:	Ulikaa (Chuo cha Dudley J. Trudge) kwa muda gani?	A:	How long did you spend at (Dudley J. Trudge College)?
B:	Nilikaa (Chuo cha Dudley J. Trudge) kwa muda wa (miaka minne).	B:	I stayed at (Dudley J. Trudge College) for a period of (four years).

C-4

A:	Ulihudhuria chuo gani?	A:	What college did you attend?
B:	Nilihudhuria chuo cha ________________.	B:	I attended ________________.
A:	Ulihudhuria chuo cha ________ kwa muda gani?	A:	How long did you attend __________?
B:	Nilihudhuria chuo cha _________ kwa muda wa ___________.	B:	I attended ___________ for a period of ____________.

C-5

A:	Watoka jimbo gani?	A:	What state are you from?
B:	Natoka jimbo la (Massachusetts).	B:	I'm from (Massachusetts).
A:	Uliishi (katika) jimbo la (Massachusetts) kwa muda gani?	A:	How long did you live in (Massachusetts)?
B:	Niliishi (Massachusetts) kwa muda wa ___________.	B:	I lived in (Massachusetts) for a period of __________.

TO THE STUDENT:

/kila/ 'each, every' is one of the few Swahili adjectives which precedes the noun.

/kilimo/ 'agriculture' is, of course, related to the verb /kulima/ 'to hoe, to work the land'. This is another example of verbs and nouns sharing the same root.

CYCLE 61

M-1

viazi	Kuna viazi.	potatoes	There are potatoes.
nyama (9)	Kuna nyama.	meat	There is meat.
mboga (9,10)	Kuna mboga.	vegetables	There are vegetables.
wali (14)	Kuna wali.	rice	There is rice.
mkate (3,4)	Kuna mkate.	bread	There is bread.
siagi (9)	Kuna siagi.	butter	There is butter.
matunda (6)	Kuna matunda.	fruit	There is fruit.

M-2

chakula (7,8)	Kuna chakula gani leo?	food	What kind of food is there today?

C-1

A: Kuna chakula gani leo?	A: What kind of food is there today?
B: Kuna (nyama).	B: There is (meat).

C-2

A: Kuna chakula gani leo?	A: What kind of food is there today?
B: Kuna (nyama) na (wali).	B: There is (meat) and (rice).

Arrange for one person in each class to be informed of the menu for the next meal. He can then announce that information at the end of the class session. Continue this practice for a week.

CYCLE 62

M-1

nyama	Nilikula nyama jana usiku.	meat	I ate meat last night.
mboga	Nilikula mboga jana usiku.	vegetables	I ate vegetables last night.
supu (9)	Nilikula supu jana usiku.	soup	I ate soup last night.

M-2

chakula	Ulikula chakula gani jana usiku?	food	What kind of food did you have (eat) last night?

M-3

kahawa (9)	Nilikunywa kahawa.	coffee	I drank coffee.
maziwa (6)	Nilikunywa maziwa.	milk	I drank milk.
maji (6)	Nilikunywa maji.	water	I drank water.
pombe (9)	Nilikunywa pombe.	beer	I drank beer.
chai (9)	Nilikunywa chai.	tea	I drank tea.

M-4

kunywa	Ulikunywa nini jana usiku?	to drink	What did you drink last night?

C-1

A:	Ulikula nini kwa chakula cha jioni jana usiku?	A:	What did you have (eat) for supper last night?
B:	Nilikula (nyama), (mboga), na (viazi).	B:	I ate (meat), (vegetables), and and (potatoes).
A:	Ulikunywa nini?	A:	And what did you drink?
B:	Nilikunywa (kahawa).	B:	I drank (coffee).

C-2

A:	Ulikunywa (kahawa) jana usiku?	A:	Did you drink (coffee) last night?
B:	Ndiyo, nilikunywa (kahawa).	B:	Yes, I drank (coffee).
	La, sikunywa (kahawa).		No, I didn't drink (coffee).
	Nilikunywa (chai).		I drank (tea).

CYCLE 63

M-1

ng'ombe	Kulikuwa na nyama ya ng'ombe jana usiku.	cow	There was beef last night.
nguruwe	Kulikuwa na nyama ya nguruwe jana usiku.	pig	There was pork last night.
kuku	Kulikuwa na kuku jana usiku.	chicken	There was chicken last night.
mbuzi	Kulikuwa na nyama ya mbuzi jana usiku.	goat	There was goat meat last night.

M-2

nyama	Kulikuwa na nyama gani?	meat	What kind of meat was there?

M-3

ndizi (9,10)	Kulikuwa na ndizi leo asubuhi.	banana	There were bananas this morning.
papai (5, 6)	Kulikuwa na mapapai leo asubuhi.	papaya	There were papayas this morning.
chungwa (5, 6)	Kulikuwa na machungwa leo asubuhi.	orange	There were oranges this morning.
embe (5, 6)	Kulikuwa na maembe leo asubuhi.	mango	There were mangoes this morning.
nanasi (5, 6)	Kulikuwa na mananasi leo asubuhi.	pineapple	There were pineapples this morning.

M-4

tunda (5, 6)	Kulikuwa na matunda gani?	fruit	What kind of fruit was there?

C-1

A:	Ulikula nyama gani jana usiku (jioni)?	A:	What kind of meat did you eat last night?
B:	Nilikula ( ).	B:	I ate ( ).
A:	Ulikula matunda gani?	A:	What kind of fruit did you eat?
B:	Nilikula ( ).	B:	I ate ( ).
	Sikula matunda jana usiku (jioni).		I didn't eat fruit last night.

C-2

A:	Kulikuwako matunda gani asubuhi leo?	A:	What kind of fruit was there this morning?
B:	Kulikuwako (ndizi) na (machungwa).	B:	There were (bananas) and (oranges).
A:	Ulikula matunda gani?	A:	What kind did you eat?
B:	Nilikula (ndizi).	B:	I ate (bananas).
A:	(Fulani), (Bw. Kanyati) alikula matunda gani leo asubuhi?	A:	(So-and-So), what kind of fruit did (Mr. Kanyati) eat this morning?
B:	(Bw. Kanyati) alikula (mapapai) leo asubuhi.	B:	(Mr. Kanyatii) ate (papayas) this morning.

C-3

A:	Ulikula nyama gani jana jioni?	A:	What kind of meat did you eat last night?
B:	Nilikula nyama ya (ng'ombe).	B:	I ate (beef).
A:	(Fulani), (Bw. Kanyati alikula nyama ya (kuku) jana jioni?	A:	(So-and-So), did (Mr. Kanyati) eat (chicken) last night?
B:	La, (Bw. Kanyati) hakula nyama ya (kuku).	B:	No, (Mr. Kanyati) didn't eat (chicken).
A:	Alikula nyama ya (ng'ombe).	A:	He/she ate (beef).

CYCLE 64

Students should be able to construct for themselves the question 'What kinds of vegetables are there?' In this way, they should learn the Swahili words for all kinds of vegetables that they have eaten within the past 48 hours.

Students should also make a list of other foods (e.g. eggs) and ask the instructor to give them the Swahili words for these foods.

C-1

A:	Ulikula nini kwa (chakula cha asubuhi), (mchana), (jioni)?	A:	What did you eat for (breakfast), (lunch), (supper)?
B:	Nilikula ( ) na ( ).	B:	I ate ( ) and ( ).[Give complete list.]
	Nilikunywa ( ).		I drank ( ).

CYCLE 65

M-1

machungwa	Machungwa yalikuwa mazuri sana.	oranges	The oranges were very good.
ndizi	Ndizi zilikuwa nzuri sana.	bananas	The bananas were very good.
nyama	Nyama ilikuwa nzuri sana.	meat	The meat was very good.
mapapai	Mapapai yalikuwa mazuri sana.	papayas	The papayas were very good.
wali	Wali ulikuwa mzuri sana.	rice	The rice was very good.
viazi	Viazi vilikuwa vizuri sana.	potatoes	The potatoes were very good.
mkate	Mkate ulikuwa mzuri sana.	bread	The bread was very good.
kahawa	Kahawa ilikuwa nzuri sana.	coffee	The coffee was very good.
maziwa	Maziwa yalikuwa mazuri sana.	milk	The milk was very good.

M-2

machungwa	Machungwa yalikuwa mazuri?	oranges	Were the oranges good?
ndizi	Ndizi zilikuwa nzuri?	bananas	Were the bananas good?
nyama	Nyama ilikuwa nzuri?	meat	Was the meat good?
maembe	Maembe yalikuwa mazuri?	mangoes	Were the mangoes good?
chai	Chai ilikuwa nzuri?	tea	Was the tea good?
viazi	Viazi vilikuwa vizuri?	potatoes	Were the potatoes good?
mkate	Mkate ulikuwa mzuri?	bread	Was the bread good?

C-1

A: Ulikula nini jana usiku?	A: What did you eat last night?
B: Nilikula (nyama) na (wali).	B: I ate (meat) and (rice).
A: (Nyama) (i)likuwa (n)zuri?	A: Was the (meat) good?
B: Ndiyo, (nyama) (i)likuwa (n)zuri sana.	B: Yes, the (meat) was very good.
A: Na (wali) je?	A: And what about the (rice)?
B: (Wali) pia (u)likuwa (m)zuri.	B: The (rice) was good also.

C-2

A:	Ulikunywa nini kwa chakula cha asubuhi leo?	A:	What did you drink for breakfast this morning?
B:	Nilikunywa (chai).	B:	I drank (tea).
A:	(I)likuwa (n)zuri?	A:	Was it good?
B:	Ndiyo, (I)likuwa (n)zuri sana.	B:	Yes, it was very good.

66 SR

Students should learn to ask and answer the question, 'Was the (food or drink) good?' for all the kinds of food or drink for which they know the names. Make a list of the nouns, followed by the form of the verb ('was') and the adjective that belongs with it.

Machungwa	yalikuwa	mazuri?	The oranges	were	good?
______	______	______	______	___	___
______	______	______	______	___	___
______	______	______	______	___	___
______	______	______	______	___	___
______	______	______	______	___	___
______	______	______	______	___	___
______	______	______	______	___	___
______	______	______	______	___	___
______	______	______	______	___	___

TEXTS SERIES TD

The Weather

Text TD-1

Hali ya hewa mjini Dar-es-Salaam katika mwezi wa Septemba si nzuri sana.	The weather in the city of Dar in the month of September is not very good.
Kuna joto kali sana na pia hewa ina unyevunyevu mwingi.	There is very much heat and also the air has much humidity.
Wakati huu ni wakati ambapo mji huwa na joto jingi kuliko wakati mwingine, na mvua huweza kuja wakati wowote.	This period is the time when the city becomes hotter than at any other period, and it may rain any time.
Na mara nyingi ukiamka asubuhi, huwezi kujua kama itanyesha au sivyo.	And on many occasions when you wake up in the morning you cannot be sure if it will rain or not.

hali (9)	condition
hewa (9)	air
hali ya hewa	weather
joto (5)	heat
kali (adj.)	fierce, sharp, cutting
mara (9, 10)	occasion
au sivyo	or not

Text TD-2

Mwezi wa Novemba joto linaanza kupungua, kwani mvua inaanza kuja.	In November the heat begins to decrease, because it begins to rain.
Na hivyo ingawa kuna unyevunyevu, hali ya hewa si joto sana.	And therefore even though there is humidity, the weather is not very hot.
Na wakati huu, matunda yanaanza kuonekana kwa wingi mjini, kwa sababu ya mvua inawezesha mimea izidi kuchipua zaidi.	And at this time fruit is seen in quantity in the city, because the rain enables the plants to sprout more [blossoms].

kupungua	to decrease
kwani	because
hivyo	in that manner, thus
ingawa	even though
matunda (6)	fruit (pl.)
kuonekana	to appear
kwa wingi	in quantity
kuwezesha	to enable
mimea (4)	plants

kuzidi	to increase
kuchipua	to sprout

Text TD-3

Mwezi wa Januari, ni bado una joto, lakini mvua inakuwa imelipunguza joto.	There is still heat in January, but the rain has reduced it.
Mvua huendelea kunyesha tu mpaka mwezi wote uishe.	It continues to rain until the month ends.
Na wakati huu matunda yanakuwa ni mengi sana mjini.	At this time, there is a lot of fruit in the city.
Lakini huwa ni bado sana mpaka wakati wa baridi.	But fruit continues to be available until the cold weather.
Na watu wa Dar wanakuwa bado wako katika taabu ya jasho.	And the people of Dar are still troubled by heat.

bado	still, yet
kupunguza	to cause to decrease
kuisha	to finish
baridi (9)	cold
taabu (9)	trouble
jasho (9)	heat

Text TD-4

Mvua mara nyingi inafika asubuhi sana katika mwezi wa Januari.	It often rains early in the morning in the month of January.
Mvua inafika mchana katika mwezi wa Machi.	It rains during the day in the month of March.
Hali ya hewa inaanza kuwa nzuri.	The weather starts to be good.
Mvua inapungua na kunakuwa na baridibaridi.	The [amount of] rain decreases and it becomes cool.
Lakini Wakati wa baridi unakuwa haujafika bado.	But the cold weather has not yet arrived.
Na wakati huu, miti inaanza kuotesha majani, na kujitayarisha na ukame wa nchi unaofuata baadaye.	At this period, the trees begin to grow leaves, and to ready themselves for the drought in the country that follows.
Na matunda hupotea mjini.	And the fruit disappears from the city.

mchana (3)	day time
baridibaridi	cool
mti (3, 4)	tree

kuotesha	to cause to grow
jani (5, 6)	leaf
kutayarisha	to make ready
ukame (14)	drought
baadaye	later
kupotea	to disappear, get lost

Text TD-5

Katika mwezi wa Mei, ni wakati wa baridi Dar.	The month of May is a cold month in Dar.
Ninaposema 'baridi' yaani baridi kufananisha na wakati mwingine.	When I say cold, that is the cold in comparison to other seasons.
Watu hutoka bado jasho.	People are still sweating.
Lakini, kwa mtu ye yote aliyepata kufika Dar-es-Salaam na kukaa mwaka mzima pale, ataona kuwa huu ni wakati wa nafuu.	But (for) anyone who has been to Dar and lived there a whole year, he will understand that this is a period of good weather.
Mvua huwa ni kidogo sana ingawa bado inanyesha.	There is very little rain although it still rains.
Na mtu anaweza kuvaa koti bila kupata taabu sana.	One can wear a coat without much trouble.

kufananisha	to compare
kufanana	to resemble
kutoka jasho	to sweat
nafuu (9)	gain, progress, advantage

Text TD-6

Mwezi wa Julai ni mwezi wa baridi pia.	July is a cold month also.
Baridi karibu inakwisha lakini bado iko.	The cold is almost gone but it is still there.
Na labda kuna baridi zaidi kuliko mwezi wa Mei.	And perhaps it is colder than May.
Wakati huu, huwa kuna vumbi karibu mjini kote kwa shauri ya pepo kali zinazotoka baharini.	At this time, it is generally dusty in almost the entire city because of the strong winds which blow from the sea.
Na hali ya hewa hii huendelea mpaka mwisho wa mwezi na pengine, hata kuendelea zaidi.	And this condition of weather continues until the end of the month and perhaps continues even longer.

shauri	plan, advice
upepo (14, 10)	wind, breeze

Text TD-7

Hali ya hewa kati ya Dar na Iringa inatofautiana sana.	The weather of Dar and of Iringa are very different from each other.
Tofauti ni hii.	This is the difference.
Inatokana na mahali miji ilipo.	It is caused by the location of the cities.
Mji wa Iringa uko juu sana katika nyanda za juu.	The town of Iringa is high up in the highlands.
Na mji wa Dar uko pwani.	And the city of Dar is on the coast.
Hivyo tukichukua mwezi wa Mei tutaona kuwa Iringa ni mji wa baridi sana.	Therefore if we take the month of May we see that Iringa is a very cold city.
Na watu hata wanahitaji makoti.	And the people even need coats.
Kumbe, Dar huwa hakuna joto.	Surprisingly, Dar is not hot.
Na watu wanaweza kuvaa mashati yao kama kawaida, ingawa kunakuwa na baridi kuliko wakati mwingine.	And people can wear their shirts as usual, although it is colder than any other time.

kutofautiana	to differ from
tofauti (9)	difference
kutokana	to originate in
mahali (16)	place, location, to carry, take
kuhitaji	to need, require
kumbe	expression of surprise

Text TD-8

Nilipokwenda mjini Nairobi, sikuchukiwa sana na hali ya hewa ya kule.	When I went to Nairobi, I was not disturbed by the climate there.
Hali ya hewa ya kule ni ya kupendeza.	The weather there is pleasant.
Ni tofauti kidogo na hali ya hewa ya Iringa ambako natoka, lakini inafanana sana.	It is a little different from the climate of Iringa where I come from, but resembles it very much.
Pana joto zaidi Nairobi kuliko Iringa.	There is more heat in Nairobi than in Iringa.
Lakini nilipokuwa pale katika mwezi wa Agosti niliona watu wanavaa makoti bila kusumbuka.	But when I was there in August I saw people wearing jackets without feeling uncomfortable.
Na Nairobi ni mji mzuri na wa kupendeza.	And Nairobi is a beautiful and pleasant town.

kuchukia	to dislike
kupendeza	to please, be pleasing
kusumbuka	to be uncomfortable

Text TD-9

Wakati wa kaskazi, Washington huwa una joto sana.	In the summer, Washington is generally very hot.
Na mtu anayefika hapa wala hawezi kuamini kuwa ni nchi iliyoko katika nchi za kaskazini za dunia.	And a person who arrives here cannot believe that it is a country which is in the northern countries of the world.
Joto huwa kali sana, na huwa unatoka jasho sana kama sehemu nyingine za tropiki.	The heat is very [intense] and you sweat very much as in some parts of the tropics.
Lakini huu ni wakati wa summer tu.	But this is only [in the] summer time.
Mtu huweza kushangaa atakavyoona hali ya hewa inavyogeuka.	One may be surprised when he sees how the weather changes.

kaskazi (9)	northerly wind, summer
wala	(negative)
kuamini	to trust, believe
dunia (9)	world
tropiki (9, 10)	tropics
kushangaa	to be surprised
kugeuka	to change, turn

Text TD-10

Wakati wa kusi mji wa Washington huwa una baridi sana.	In the winter time the city of Washington is very cold.
Yaani ukifananisha na wakati wa kaskazi utaona tofauti kubwa sana.	That is, if you compare it with summer time, you will see a big difference.
Wakati fulani theluji inaanguka na hata magari hayawezi kutembea vizuri mpaka theluji iondolewe barabarani.	At certain times snow falls and [even] cars cannot run well until the snow is removed from the road.
Na joto linashuka mpaka zero au chini zaidi, na kwa jumla, hali ya hewa, huwa si ya nafuu mpaka ukae katika nyumba iliyo na mashine za kuweza kutoa joto au ukoke moto.	The temperature drops down to zero or less and generally, the weather is not good (healthy) unless you stay in a house which has a machine which gives heat or you make a fire.
Na magari pia, lazima yawe na mashine ya kutolea joto.	And cars too, have to have a machine for (giving out) heat.

kusi (9)	southerly wind, winter
theluji (9)	snow
kuanguka	to fall, drop
kushuka	to lower, descend
chini (9)	below, bottom
jumla (9)	sum, total
mashine (9, 10)	machine
kutoa	to diffuse, give (off)
kukoka	to build a fire
moto (3, 4)	flame, fire
lazima	necessity, obligation

CYCLE 67

For this lesson and the ones that follow it, the teacher will need the following things:

- 3 large pens and/or pencils
- 3 small pens and/or pencils
- 3 large books
- 3 small books
- 3 large hard boiled eggs
- 3 small hard boiled eggs
- 3 large nails
- 3 small nails
- 3 small pieces of paper
- 3 large pieces of paper

The students should bring these things to class for the use of the teacher.

The Instructor should place on the table:

- 1 pen/pencil
- 1 book
- 1 egg
- 1 nail
- 1 piece of paper

M-1

kalamu ya wino (au kalamu) (9, 10)	Hiyo ni kalamu ya wino/kalamu.	pen/pencil	That is a pen/pencil.
kitabu (7, 8)	Hicho ni kitabu.	book	That is a book.
yai (5, 6)	Hilo ni yai.	egg	That is an egg.
msumari (3, 4)	Huo ni msumari.	nail	That is a nail.
kipande cha karatasi	Hicho ni kipande cha karatasi.	paper	That is a (piece of) paper.

M-2

kitu	Hiki ni kitu gani?	thing	What is this?

C-1

A: Hiki ni kitu gani?	A: What is this?
B: Hi(lo) ni (yai).	B: This is (an egg).

CYCLE 68

The instructor should place on the table:

- 2 nails
- 2 books
- 2 pieces of paper
- 2 eggs
- 2 pens/pencils

M-1

misumari	Hiyo ni misumari.	nails	Those are nails.
vitabu	Hivyo ni vitabu.	books	Those are books.
vipande vya karatasi	Hivyo ni vipande vya karatasi.	pieces of paper	Those are pieces of paper.
mayai	Hayo ni mayai.	eggs	Those are eggs.
kalamu	Hizo ni kalamu.	pens	Those are pens.

C-1

A: Hivi ni vitu gani?	A: What are these?
B: Ni (vitabu).	B: They are (books).

C-2

A: Hiki ni kitu gani?	A: What is this? (pointing at one thing)
B: Ni (kitabu).	B: It's a (book).
A: Hivi ni vitu gani?	A: And what are these? (pointing at two things of the same kind)
B: Ni (kalamu).	B: They are (pens).

Remember that students should have plenty of opportunity to practice both Role A and Role B in C-1 and C-2.

CYCLE 69

M-1

kitabu kimoja	Kuna kitabu kimoja juu ya meza.	one book on the table	There's one book on the table.
vitabu viwili	Kuna vitabu viwili juu ya meza.	two books	There are two books on the table.
yai moja	Kuna yai moja juu ya meza.	one egg	There is one egg on the table.
mayai mawili	Kuna mayai mawili juu ya meza.	two eggs	There are two eggs on the table.
msumari mmoja	Kuna msumari mmoja juu ya meza.	one nail	There is one nail on the table.
misumari miwili	Kuna misumari miwili juu ya meza.	two nails	There are two nails on the table.
kalamu (ya wino) moja	Kuna kalamu ya wino moja juu ya meza.	one pen	There is one pen on the table.
kalamu (za wino) mbili	Kuna kalamu za wino mbili juu ya meza.	two pens	There are two pens on the table.
kipande cha karatasi	Kuna kipande cha karatasi mezani.	one piece of paper	There is one (piece of) paper on the table.
vipande viwili vya karatasi	Kuna vipande viwili vya karatasi mezani.	two pieces of paper	There are two (pieces of) paper on the table.

M-2

gani	Kuna kitu gani mezani? Kuna vitu gani mezani?	what	What is there on the table?

C-1

A: Kuna (kitu) gani mezani?	A: What is there on the table?
B: Kuna (yai moja) juu ya meza/mezani.	B: There's (an egg) on the table.
A: Kuna (vitu) gani mezani?	A: What is there on the table?
B: Kuna (mayai mawili) juu ya meza/mezani.	B: There are (two eggs) on the table.

CYCLE 70

M-1

1. Have the students repeat these phrases.
2. Give the nouns only. Students are to reply by giving the noun with a number.

msumari mmoja	yai moja	one nail	one egg
misumari miwili	mayai mawili	two nails	two eggs
misumari mitatu	mayai matatu	three nails	three eggs
misumari minne	mayai manne	four nails	four eggs
misumari mitano	mayai matano	five nails	five eggs
misumari sita	mayai sita	six nails	six eggs
misumari saba	mayai saba	seven nails	seven eggs
misumari minane	mayai manane	eight nails	eight eggs
misumari tisa	mayai tisa	nine nails	nine eggs
misumari kumi	mayai kumi	ten nails	ten eggs
misumari kumi na mmoja	mayai kumi na moja	eleven nails	eleven eggs
misumari kumi na miwili	mayai kumi na mawili	twelve nails	twelve eggs

kitabu kimoja	kalamu moja	one book	one pen
vitabu viwili	kalamu mbili	two books	two pens
vitabu vitatu	kalamu tatu	three books	three pens
vitabu vinne	kalamu nne	four books	four pens
vitabu vitano	kalamu tano	five books	five pens
vitabu sita	kalamu sita	six books	six pens
vitabu saba	kalamu saba	seven books	seven pens
vitabu vinane	kalamu nane	eight books	eight pens
vitabu tisa	kalamu tisa	nine books	nine pens
vitabu kumi	kalamu kumi	ten books	ten pens
vitabu kumi na kimoja	kalamu kumi na moja	eleven books	eleven pens
vitabu kumi na viwili	kalamu kumi na mbili	twelve books	twelve pens

C-1

A:	Msumari mmoja na msumari mmoja ni misumari mingapi?	A:	One nail and one nail are how many nails?
B:	Msumari mmoja na msumari mmoja ni misumari miwili.	B:	One nail and one nail are two nails.
A:	Mayai matatu na mayai matano ni mayai mangapi?	A:	Three eggs and five eggs are how many eggs?
	(Na kadhalika)		(etc.)

CYCLE 71

M-1

In this lesson the class will need a large box and a sack or bag.

meza (9,10)	Sasa, kuna misumari miwili juu ya meza.	table	Now, there are two nails on the table.
sakafu (9)	Sasa, kuna misumari miwili juu ya sakafu.	floor	Now, there are two nails on the floor.
sanduku (5,6) or (9,10)	Sasa, kuna misumari miwili ndani ya sanduku.	box	Now, there are two nails in the box.
gunia (5,6)	Sasa, kuna misumari miwili ndani ya gunia.	sack	Now, there are two nails in the sack.

M-2

meza	Kulikuwa na misumari mitatu juu ya meza.	table	There were three nails on the table.
sakafu	Kulikuwa na misumari mitatu juu ya sakafu.	floor	There were three nails on the floor.
sanduku	Kulikuwa na misumari mitatu ndani ya sanduku.	box	There were three nails in the box.
gunia	Kulikuwa na misumari mitatu ndani ya gunia.	bag	There were three nails in the box.

C-1

The teacher, or the student who is asking the questions, should place a certain number of articles on the floor or on the table or in a box or a bag, as he talks.

A:	Kuna (misumari mi)ngapi (juu ya meza)?	A:	How many (nails) are there (on the table)?
B:	Kuna (misumari mitatu) (juu ya meza).	B:	There are (three nails) (on the table).

C-2

A:	Kuna (misumari mi)ngapi juu ya (sakafu)?	A:	How many (nails) are there on the (floor)?
B:	Kuna (misumari mitatu) juu ya (sakafu).	A:	There are (three nails) on the (floor).

The person who asked the question adds one more object, or takes away one object. The person who answered the question must now say:

B:	Kulikuwa na (misumari mitatu) juu ya (sakafu),	B:	There were (three nails) on the (floor),
	lakini sasa kuna (misumari minne) juu ya (sakafu).		but now there are (four) on the (floor).

CYCLE 72

In Cycles 67 through 71, the size of the objects was not important. In this cycle, difference in size is important.

M-1

msumari	Msumari mmoja mkubwa na misumari miwili midogo ni misumari mitatu.	nail	One large nail and two small nails are three nails.
yai	Yai moja kubwa na mayai mawili madogo ni mayai matatu.	egg	One large egg and two small eggs are three eggs.
kitabu	Kitabu kikubwa kimoja na vitabu viwili vidogo ni vitabu vitatu.	book	One large book and two small books are three books.
kalamu	Kalamu kubwa moja na kalamu mbili ndogo ni kalamu tatu.	pencil	One large pencil and two small pencils are three pencils.

M-2

Tafadhali nipe misumari miwili mikubwa na msumari mmoja mdogo.	Please hand me two large nails and one small nail.
Tafadhali nipe mayai mawili makubwa na yai moja dogo.	Please hand me two large eggs and one small egg.
Tafadhali nipe vitabu viwili vikubwa na kitabu kimoja kidogo.	Please hand me two large books and one small book.
Tafadhali nipe kalamu mbili kubwa na kalamu moja ndogo.	Please hand me two large pens and one small pen.

C-1

Tafadhali nipe (mayai mawili makubwa na yai moja dogo).	Please hand me (two large eggs and one small egg).

C-2

A: (Chicago) ni (mji m)kubwa au (m)dogo?	A: Is (Chicago) large, or small?
B: Ni (mkubwa)	B: It is (large).

C-3

A: (Chumba chako) ni (ki)kubwa au (ki)dogo?	A: Is (your room) large, or small?
B: Ni (kikubwa).	B: It's (large).

CYCLE 73

M-1

msumari	Chukua misumari mitatu.	nail	Take three nails.
kitabu	Chukua vitabu vitatu.	book	Take three books.
yai	Chukua mayai matatu.	egg	Take three eggs.
kalamu	Chukua kalamu tatu.	pencil	Take three pencils.

M-2

vitabu	Weka kitabu kimoja sandukuni.	books	Put one book in the box.
kalamu	Weka kalamu moja sandukuni.	pencils	Put one pencil in the box.
mayai	Weka yai moja sandukuni.	eggs	Put one egg in the box.
msumari	Weka msumari mmoja sandukuni.	nails	Put one nail in the box.

C-1

> The teacher should give instructions to the students. Later, the students themselves should give instructions. Some examples are:

Chukua misumari mikubwa miwili. Weka msumari mmoja juu ya meza.	Take two large nails. Put one nail on the table.
Chukua misumari mikubwa mitatu na midogo miwili. Weka msumari mmoja sakafuni.	Put one nail on the floor. Take three large nails and two small ones.
Weka misumari mikubwa sandukuni. Weka midogo mezani.	Put the large nails in the box. Put the small ones on the table.

[Some speakers may prefer the verb /tia/ in place of /weka/ in the above sentences.]

CYCLE 74

M-1

kalamu	Rudisha kalamu mezani.	pencils	Return the pencils to (on) the table.
mayai	Rudisha mayai mezani.	eggs	Return the eggs to (on) the table.
vitabu	Rudisha vitabu mezani.	books	Return the books to (on) the table.
misumari	Rudisha misumari mezani.	nails	Return the nails to (on) the table.

M-2

kalamu	Kalamu ziko wapi sasa?	pens	Where are the pens now?
vitabu	Vitabu viko wapi sasa?	books	Where are the books now?
mayai	Mayai yako wapi sasa?	eggs	Where are the eggs now?
misumari	Misumari iko wapi sasa?	nails	Where are the nails now?

C-1

> The person who gives the instructions to one person also asks questions of another person.

A: Weka vitabu vitatu mezani.	A: Put three books on the table. [B carries out the order.]
A: Vitabu viko wapi?	A: Where are the books?

C: Vitabu viko mezani.	C: The books are on the table.
A: Rudisha vitabu katika gunia.	A: Return the books to the sack.
A: Vitabu viko wapi sasa?	A: Where are the books now?
(N.K.)	(etc.)

CYCLE 75

M-1

msumari	Chukua msumari mmoja. Uweke juu ya meza.	nail	Take one nail. Put it on the table.
misumari	Chukua misumari miwili. Iweke juu ya meza.	nails	Take two nails. Put them on the table.
yai	Chukua yai moja. Liweke juu ya meza.	egg	Take one egg. Put it on the table.
mayai	Chukua mayai mawili. Yaweke juu ya meza.	eggs	Take two eggs. Put them on the table.
kitabu	Chukua kitabu kimoja. Kiweke juu ya meza.	book	Take one book. Put it on the table.
vitabu	Chukua vitabu viwili. Viweke juu ya meza.	books	Take two books. Put them on the table.
kalamu	Chukua kalamu moja. Iweke juu ya meza.	pencil	Take one pencil. Put it on the table.
kalamu	Chukua kalamu mbili. Ziweke juu ya meza.	pencils	Take two pencils. Put them on the table.

M-2

msumari	Nilichukua msumari mmoja nikauweka juu ya meza.	nail	I took one nail and put it on the table.
misumari	Nilichukua misumari miwili nikaiweka juu ya meza.	nails	I took two nails and put them on the table.
yai	Nilichukua yai moja nikaliweka juu ya meza.	egg	I took one egg and put it on the table.
mayai	Nilichukua mayai mawili nikayaweka juu ya meza.	eggs	I took two eggs and put them on the table.

kitabu	Nilichukua kitabu kimoja nikakiweka juu ya meza.	book	I took one book and put it on the table.
vitabu	Nilichukua vitabu viwili nikaviweka juu ya meza.	books	I took two books and put them on the table.
kalamu	Nilichukua kalamu moja nikaiweka juu ya meza.	pencil	I took one pencil and put it on the table.
kalamu	Nilichukua kalamu mbili nikaziweka juu ya meza.	pencils	I took two pencils and put them on the table.

C-1

A: Chukua (vitabu viwili).	A: Take (two books). [B does so.]
A: (Vi)weke juu ya (meza).	A: Put (them) (on the table).
A: Ulifanya nini?	A: What did you do?
B: Nilichukua (vitabu viwili) nika(vi)weka juu ya (meza).	B: I took (two books) and put them (on the table).

C-2

A: Chukua (mayai manne). Yatie (mezani).	A: Take (four eggs). Put them (on the table).
A: B alifanya nini?	A: What did B do?
C: Alichukua (mayai manne) ya aka(ya)weka (mezani).	C: He/she took (four eggs) and put (them) (on the table).

CYCLE 76

M-1

msumari	Msumari huu ni mkubwa; msumari huo ni mdogo.	nail	This nail is big; that nail is little.
misumari	Misumari hii ni mikubwa; misumari hiyo ni midogo.	nails	These nails are big; those nails are small.
yai	Yai hili ni kubwa; yai hilo ni dogo.	egg	This egg is big; that egg is small.
mayai	Mayai haya ni makubwa; mayai hayo ni madogo.	eggs	These eggs are big; those eggs are small.
kitabu	Kitabu hiki ni kikubwa; kitabu hicho ni kidogo.	book	This book is big; that book is little.

vitabu	Vitabu hivi ni vikubwa; vitabu hivyo ni vidogo.	books	These books are big; those books are little.

C-1

A: (Yai) h(ili) ni kubwa au dogo?	A: Is this (egg) big, or little?
B: Ni (dogo).	B: It is (big).

C-2

A: (Misumari) h(iyo) ni (mi)kubwa au (mi)dogo?	A: Are these (nails) big, or little?
B: Ni (midogo).	B: They are (little).

C-3

A: (Kitabu) h(ich)o ni (ki)kubwa au (ki)dogo?	A: Is that (book) big, or little?
B: Ni (kikubwa).	B: It is (large).

C-4

A: (Misumari) h(iy)o ni (mi)kubwa au (mi)dogo?	A: Are those (nails) big, or little?
B: Ni (mikubwa).	B: They are (big).

CYCLE 77

M-1

mimi	Tafadhali nipe vitabu.	me	[Please] hand me the books.
Daudi	Tafadhali mpe Daudi vitabu.	David	[Please] hand David the books.
Daudi na Maria	Tafadhali wape Daudi na Maria vitabu.	David and Mary	[Please] hand David and Mary the books.
Daudi na mimi	Tafadhali tupe (mimi na Daudi) vitabu.	David and me	[Please] hand David and me the books.

M-2

mimi	Daudi alinipa pesa.	me	David gave me some money.
wewe	Daudi alikupa pesa.	you (sg.)	David gave you some money.
wewe na mimi	Daudi alitupa pesa.	you (sg.) and me	David gave you and me some money.
wewe na Maria	Daudi aliwapeni pesa.	you (sg.) and Mary	David gave you and Mary some money.
Maria na Yohana	Daudi aliwapa Maria na Yohana pesa.	Mary and John	David gave Mary and John some money.

C-1

A: (Wa)pe (Daudi na Maria) (vitabu vitano).	A: Give (five books) to (David and Mary). [B does so.]
A: Ulifanya nini?	A: What did you do?
B: Nili(wa) pa (Daudina Maria) (vitabu vitano).	B: I gave (five books) to (David and Mary).
A: (B) alifanya nini?	A: What did (B) do?
C: Ali(wa) pa (Daudi na Maria) (vitabu vitano).	C: He/she gave (five books) to (David and Mary).

CYCLE 78

M-1

shati (5,6)	Shati la John ni la rangi gani?	shirt	What color is John's shirt?
kaptura (9,10)	Kaptura ya John ni ya rangi gani?	shorts	What color are John's shorts?
suruali (9, 10)	Suruali ya John ni ya rangi gani?	long trousers	What color are John's trousers?
soksi (9,10)	Soksi za John ni za rangi gani?	socks	What color are John's socks?
viatu (8)	Viatu vya John ni vya rangi gani?	shoes	What color are John's shoes?
kofia (9,10)	Kofia ya John ni ya rangi gani?	hat	What color is John's hat?
vazi (5,6)	Vazi la Mary ni la rangi gani?	dress	What color is Mary's dress?

M-2

nyekundu	Vazi la Mary ni jekundu.	red,brown	Mary's dress is red.
nyeupe	Vazi la Mary ni jeupe.	white	Mary's dress is white.
nyeusi	Vazi la Mary ni jeusi.	black	Mary's dress is black.
kijanibichi or: kijani kibichi	Vazi la Mary ni la kijanibichi.	green	Mary's dress is green.
kibluu or: kibuluu	Vazi la Mary ni la kibluu.	blue	Mary's dress is blue.
kisamawati	Vazi la Mary ni la kisamawati.	light blue	Mary's dress is light blue.
njano	Vazi la Mary ni la njano.	yellow	Mary's dress is yellow.

M-3

nyekundu	Viatu vya Mary ni vyekundu.	red	Mary's shoes are red.
nyeupe	Viatu vya Mary ni vyeupe.	white	Mary's shoes are white.
nyeusi	Viatu vya Mary no vyeusi.	black	Mary's shoes are black.
kijanibichi or: kijani kibichi	Viatu vya Mary ni vya kijanibichi.	green	Mary's shoes are green.
kibluu	Viatu vya Mary ni vya kibluu.	blue	Mary's shoes are blue.
samawati	Viatu vya Mary ni vya samawati.	light blue	Mary's shoes are light blue.
njano	Viatu vya Mary ni vya njano.	yellow	Mary's shoes are yellow.

C-1

[Ask and answer questions about the colors of books, clothing, pens, etc inside the classroom. Be sure to use the correct form of the color word, so that it agrees with the noun.]

CYCLE 79

M-1

kalamu	Kalamu hii ni ya nani?	pencil	Whose pencil is this?
karatasi	Karatasi hii ni ya nani?	paper	Whose paper is this?
kiberiti	Kiberiti hiki ni cha nani?	matches	Whose matches are these?
saa	Saa hii ni ya nani?	watch	Whose watch is this?
kiti	Kiti hiki ni cha nani?	chair	Whose chair is this?

M-2

mimi	Kalamu hizi ni zangu.	I	These pencils are mine.
wewe	Kalamu hizi ni zako.	you (sg.)	These pencils are yours.
yeye	Kalamu hizi ni zake.	he/she	These pencils are his/hers.
sisi	Kalamu hizi ni zetu.	we	These pencils are ours.
ninyi	Kalamu hizi ni zenu.	you (pl.)	These pencils are yours.
wao	Kalamu hizi ni zao.	they	These pencils are theirs.

C-1

A: (Karatasi hii) ni ya nani?	A: Whose (paper) is this?
B: Ni (karatasi) (yake).	B: It is (his/hers).
A: (Kalamu) hizi ni za nani?	A: Whose (pencils) are these?
B: Ni (kalamu) (zangu).	B: They are (mine).

CYCLE 80

M-1

sufi (9)	Shati la John ni la sufi.	wool	John's shirt is made of wool.
pamba (9)	Shati la John ni la pamba.	cotton	John's shirt is made of cotton.
kitani	Shati la John ni la kitani.	linen	John's shirt is made of linen.
nylon	Shati la John ni la nylon.	nylon	John's shirt is made of nylon.

M-2

nini?	Shati la John ni la nini?	what?	What is John's shirt made of?

C-1

A:	(Shati) (l)a (John) ni (l)a nini?	A:	What is (John's) (shirt) [made] of?
B:	Ni (l)a (pamba).	B:	It's [made] of (cotton).
A:	Na ni (l)a rangi gani?	A:	And what color is it?
B:	Ni (jeupe).	B:	It's (white).

CYCLE 81

For this cycle, the class will need six empty paper cups. Pretend that one cup is full of water, another is full of coffee, etc. Write on the cups the words water, coffee, sugar, salt, milk, tea.

M-1

maji (6)	Maji yamemwagika.	water	The water is spilt.
